

102/3

KISWAHILI

KARATASI LA TATU

JULAI/AGOSTI 2012

SAA: 2½

TATHMINI YA PAMOJA WILAYA KISUMU MASHARIKI NA KASKAZINI

Kenya Certificate of Secondary Education (K.C.S.E) 2012

102/3

KISWAHILI

KARATASI LA TATU

JULAI/AGOSTI 2012

SAA: 2½

MAAGIZO

- ❖ Jibu maswali *manne pekee*
- ❖ Swali la kwanza ni la **lazima**
- ❖ Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu **nne zilizobaki** yaani hadithi fupi, riwaya, tamthilia na fasihi simulizi
- ❖ Usijibu maswali mawili kutoka katika **sehemu moja**

SWALI LA LAZIMA

USHAIRI

1. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo

MKULIMA NA UZIMA

Mkono wa mkulima, ni mgumu kama chuma

Chakula cha mkulima, ni maharage na sima
Mtazame mkulima, hapendezi hana dhima –
Bali huyu mkulima, ndiye chanzo cha uzima

Maisha ya mkulima, ni ya dhiki na nakama
Kibanda cha mkulima, huvuja na kutetema
Mgongo wa mkulima, daima umeinama
Bali huyu mkulima, ndiye mama wa uzima

Mke wake mkulima, si wa pambo, wa huduma
Huyu mke mkulima, hana muda wa kusoma
Halalami mkulima, hunywa maji ya kisima
Bali huyu mkulima, ndiye nguzo ya uzima

Nafasi ya mkulima, aghalabu ni ya nyuma
Magarini mkulima, hadhi yake kusimama
Hadharani mkulima, huambiwa hana jema
Bali huyu mkulima, ndiye nguvu ya uzima

Elimu ya mkulima, si kusoma si kupima
Lugha yake mkulima, si kizungu ni ya mama
Sayansi ya mkulima, kupanda nyanya na nduma
Bali huyu mkulima, ndiye raha ya uzima

Hunyanyaswa mkulima, ofisi akijitoma
Anabezwa mkulima, na watu waliosoma
Akiumwa mkulima, hata dawa wamnyima !
Bali huyu mkulima, ndiye ngao ya uzima

Huyo ndiye mkulima, mjueni mkulima
Akigoma mkulima, nani atakayepuma?
Namsifu mkulima, adhaniwaye wa nyuma
Kumbe huyu mkulima, ndiye chanzo cha uzima.

- a) Eleza dhamira ya shairi hili (alama 2)
- b) Taja na kueleza mikondo yoyote miwili inayojitokeza katika shairi hili. (alama 4)
- c) Taja na kueleza mbinu zozote tatu za lugha zinazojitokeza katika shairi hili (alama 6)
- d) Andika ubeti wa pili kwa lugha nathari (alama 4)
- e) Eleza maana ya msamiati ufuatao (alama 4)
 - i). Anabezwa.
 - ii). Akijitoma
 - iii). Atakayepuma
 - iv). Hadhi

SEHEMU A

HADITHI FUPI

Mayai waziri wa maradhi na hadithi nyingine

2. “Karibu ndugu yangu waumini ni kukirimiana tunashukuru, alhamdulillah sifa zote ni zake Maulana
- a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
 - b) Wahusika hawa walikirimiana vipi? (alama 12)
 - c) “Kukirimiana” huko kulikuwa na hasara gani? (alama 4)

au

3. Adui ya mwanamke ni mwanamke Eleza kauli hii ukirejelea hadithi ya ngome ya nafsi na uteuzi wa moyoni. (alama 20)

SEHEMU B

RIWAYA

UTENGANO :SAID. A. MOHAMMED.

4. “Kuna heri gani kuonana na kisabaluu huyu uso wa kifuu”
- a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
 - b) Eleza umuhimu wa mzungumzaji. (alama 8)
 - c) Kulingana na maoni ya mzungumzaji, mrejelewa ana dosari Thibitisha. (alama 8)

au

5. a) Vita dhidi ya ubabadume vimepamba moto. Thibitisha kwa kurejelea riwaya ya utengano (alama 10)
- b) Eleza madhara yanayotokana na ubabadume kwa mujibu wa riwaya ya utengano (alama 10)

SEHEMU C

TAMTHILIA

KIFO KISIMANI: KITHAKA WA MBERIA

6. “Vitisho havitaua ndoto yetu
Nyoyo zetu zimechoka. Utawala mbaya”
- a) Fafanua muktadha wa dondoo hili (alama 4)
 - b) Kwa kurejelea dondoo hili eleza sifa mbili za msemaji (alama 2)
 - c) Thibitisha ukweli kuwa utawala wa mtemi Bokono ni utawala mbaya. (alama 14)

SEHEMU D

FASIHI SIMULIZI

7. a) Fafanua kikamilifu dhana zifuatazo za fasihi simulizi

- i) Nyiso (alama 2)
- ii) Mbolezi (alama 2)
- iii) Hodiya (alama 2)
- iv) Bembelezi (alama 2)
- v) Sifo (alama 2)

- b) i) Miviga ni nini (alama 2)
- ii). Orodhesha sherehe nne za jamii yako zinazohusishwa na miviga (alama 4)
- iii). Je, miviga ina upungufu gani (alama 4)